NKINGA REFERRAL HOSPITAL
P. O. BOX 1.
NKINGA,
TABORA –TANZANIA (E.A)

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Hospitali ya Rufaa ya Nkinga inamilikiwa na "The Free Pentecostal Church of Tanzania". Hospitali hii ipo Nkinga Wilaya ya Igunga mkoani Tabora pembezoni mwa barabara kuu itokayo Mwanza kwenda Dodoma – Dar Es Salaam kwa umbali wa Km 21 toka barabarani.

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021 hospitali imetenga fedha kwa ajili ya kuajiri wafanyakazi wapya wa kada mbalimbali ili kuwezesha utekelezaji wa mpango mkakati wa hospitali wa miaka tano 2020-2024 unaolenga kuboresha huduma za afya na kuongeza upatikanaji wa huduma za afya kwa jamii ya kanda ya Magharibi. Katika tangazo hili kuna nafasi za kazi za Kuajiriwa na nafasi za Ajira ya kujitolea kama ifuatavyo:

## 1. Nafasi za ajira za kuajiriwa

Watakaoajiriwa katika nafasi hizi watalipwa mshahara kwa kuzingatia Muundo wa Mishahara ya Serikali.

### 1.1 Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake II ( Obstetric and Gynaecology II) - Nafasi 1

**Kazi na Majukumu**

i. Kufanya kazi zote za matibabu ya wagonjwa hospitalini kulingana na taaluma yake.
ii. Kupanga, kusimamia, na kutathmini utoaji huduma katika idara yake.
iii. Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa katika eneo lake la kazi.
iv. Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya taluma yako.
v. Kufundisha wafanyakazi walio chini yake, Madakatari tarajali na kufanya utafiti wa .

**Sifa za Mwombaji**

i. Awe amehitimu shahada ya uzamili ya udaktari Bingwa wa magonjwa ya wanawake(Mmed Obstetric and Gynaecology) kutoka katika vyuo vikuu vinavyotambulika na serikali.
ii. Awe amesajiliwa na baraza la Madaktari Tanganyika.
iii. Awe na uzoefu wa kazi wa mwaka mmoja na kuendelea.
iv. Awe Raia wa Tanzania.
v. Awe ana ujuzi wa kutumia kompyuta.

### 1.2 Daktari Bingwa Magonjwa ya Ndani II (Physician II)- Nafasi 2

**Kazi na Majukumu**

i. Kufanya kazi zote za matibabu ya wagonjwa hospitalini kulingana na taaluma yake.
ii. Kupanga, kusimamia, na kutathmini utoaji huduma katika idara yake.
iii. Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa katika eneo lake la kazi.
iv. Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya taaluma yako.
v. Kufundisha wafanyakazi walio chini yake, Madaktari tarajali na kufanya utafiti wa kitabibu.



KNY MKURUGENZI MTENDAJI
HOSPITALI YA RUFAA NKINGA
S. L. P 1, NKINGA
TABORA

**Sifa za Mwombaji**

i. Awe na shahada ya uzamili ya udaktari Bingwa wa magonjwa ya Ndani (Mmed Internal Medicine) kutoka katika vyuo vikuu vinavyotambulika na serikali.
ii. Awe amesajiliwa na baraza la Madaktari Tanganyika.
iii. Awe na uzoefu wa kazi wa mwaka mmoja na kuendelea.
iv. Awe Raia wa Tanzania.
v. Awe ana ujuzi wa kutumia kompyuta

**1.3 Daktari Bingwa wa Masikio, Pua na Koo II (ENT Specialist II) – Nafasi 1**

**Kazi na Majukumu**

i. Kufanya kazi zote za matibabu ya wagonjwa hospitalini wenye magonjwa mbalimbali ya taaluma yake.
ii. Kupanga, kusimamia, na kutathmini utoaji huduma katika idara yake
iii. Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa katika eneo lake la kazi.
iv. Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya taaluma yako.
v. Kufundisha wafanyakazi walio chini yake, Madakatari tarajali na kufanya utafiti wa kitabibu.

**Sifa za Mwombaji**

i. Awe na shahada ya uzamili ya udaktari Bingwa wa magonjwa ya Ndani(Mmed ENT) kutoka katika vyuo vikuu vinavyotambulika na serikali.
ii. Awe amesajiliwa na baraza la Madaktari Tanganyika.
iii. Awe na uzoefu wa kazi wa angalau mwaka mmoja na kuendelea.
iv. Awe Raia wa Tanzania.
v. Awe ana ujuzi wa kutumia kompyuta

**1.4 Daktari Bingwa wa Usingizi II /Daktari Msaidizi wa Usingizi II (Mmed Anaesthesiology II/ AMO Anaesthesiology II)**

**Kazi na Majukumu**

vi. Kufanya kazi zote za matibabu ya wagonjwa hospitalini wenye magonjwa mbalimbali ya taaluma yake.
vii. Kupanga, kusimamia, na kutathmini utoaji huduma katika idara yake.
viii. Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya taaluma yako.
ix. Kufundisha wafanyakazi walio chini yake, Madakatari tarajali na kufanya utafiti wa kitabibu. kubaini mbinu mpya za matababu ya taaluma yake kwa wagonjwa na jamii kwa ujumla.

**Sifa za Mwombaji**

i. Awe na shahada ya uzamili ya udaktari Bingwa wa matibabu na usingizi au Stashahada ya juu ya usingizi (Mmed Anaesthesiology/ AMO Anaesthesiology) kutoka katika vyuo vikuu vinavyotambulika na serikali.
ii. Awe amesajiliwa na baraza la Madatari Tanganyika.
iii. Awe na uzoefu wa kazi wa angalau mwaka mmoja na kuendelea.
iv. Awe Raia wa Tanzania.
v. Awe ana ujuzi wa kutumia kompyuta.



KNY MKURUGENZI MTENDAJI
HOSPITALI YA RUFAA NKINGA
S. L. P 1, NKINGA
TABORA

**1.4 Daktari wa Kinywa na Meno II ( Dental Surgeon/Dentist II)- Nafasi 1**

**Kazi Na Majukumu**

i. Kufanya kazi za matibabu ya magonjwa yanayohusiana na kinywa na meno.
ii. Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma katika fani yake.
iii. Kupanga, Kusimamia na kutathmini mipango ya huduma za afya katika idara yake

**Sifa za Mwombaji**

i. Awe na Shahada ya udaktari wa Kinywa na Meno kuttoka katika vyuo vikuu vinavyotambulika na serikali.
ii. Awe amemaliza mafunzo ya mwaka mmoja ya interniship.
iii. Awe amepata usaji kamili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika.
iv. Awe na uzoefu wa kazi wa mwaka 1 na kuendelea.
v. Awe Raia wa Tanzania.
vi. Awe anaujuzi wa kutumia kompyuta.

**1.5 Afisa Muuguzi II( Nursing Officer II)- Nafasi 2**

**Kazi na Majukumu**

i. Kutoa huduma za afya na kinga kwa wagonjwa na wateja hospitalini.
ii. Kutoa ushauri Nasaha kwa wagonjwa na wateja.
iii. Kutayarisha mpango kazi wa huduma za uuguzi na kusimamia utekelezaji.
iv. Kufundisha na kufanya utafiti unaolenga kuboresha huduma za uuguzi, 5S na IPC

**Sifa za Mwombaji**

i. Awe na shahada ya kwanza ya Uuguzi kutoka vyuo vikuu vinavyotambulika na serikali na awe amehitimu mafunzo ya mwaka mmoja ya Intership.
ii. Awe amesajiliwa na Baraza la Wauuguzi na Wakunga Tanzania.
iii. Awe raia wa Tanzania
iv. Awe na uzoefu wa kazi wa miaka 3 na kuendelea.
v. Awe ana ujuzi wa kutumia kompyuta.

**1.6 Afisa Muuguzi Msaidizi II ( Assistant Nursing Officer II)- Nafasi 3**

**Kazi na Majukumu**

v. Kutoa huduma za uuguzi kwa wagonjwa na wateja hospitalini
vi. Kutoa elimu ya afya na ushauri Nasaha kwa wagonjwa na wateja.
vii. Kutayarisha mpango kazi wa huduma za uuguzi na kusimamia utekelezaji
viii. Kufundisha wafanyakazi wenzake pamoja na wanafunzi.

**Sifa za Mwombaji**

i. Awe amehitimu stashahada ya Uuguzi kutoka vyuo vinavyotambulika na serikali.
ii. Awe amesajiliwa na Baraza la Wauuguzi na Wakunga Tanzania
iii. Awe raia wa Tanzania
iv. Mwenye Uzoefu wa kuhudumia wagonjwa mahututi (Critical care) atafikiriwa zaidi
v. Awe na uzoefu wa kazi wa miaka 3 na kuendelea.
vi. Awe ana ujuzi wa kutumia kompyuta.



KNY MKURUGENZI MTEND
HOSPITALI YA RUFAA NKI
S. L. P. NKINGA
TABORA

**1.7 Muuguzi wa Usingizi II(Nurse Anaesthesit II)- Nafasi 2**

**Kazi na Majukumu**

ix. Kutoa huduma za usingizi na matibabu kwa wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo.
x. Kutoa elimu ya afya na ushauri Nasaha kwa wagonjwa na wateja.
xi. Kutayarisha mpango kazi wa huduma za usingizi na kusimamia utekelezaji
xii. Kufundisha wafanyakazi wenzake na wanafunzi wa uuguzi.

**Sifa za Mwombaji**

vii. Awe amehitimu shahada au stashahada ya Uuguzi pamoja na mafunzo ya usingizi ya mwaka mmoja na kuendelea katika fani ya usingizi kutoka vyuo vinavyotambulika na serikali.
viii. Awe amesajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.
ix. Awe Raia wa Tanzania.
x. Awe na uzoefu wa kazi wa miaka 2 na kuendelea.
xi. Awe ana ujuzi wa kutumia kompyuta.

**1.8 Afisa Mteknolojia Maabara II – Nafasi 2**

**Kazi na Majukumu**

i. Kufanya kazi za uchunguzi wa kimaabara katika maeneo mbalimbali (Haematology, Parasitology, Microbiology, Immunology, Serology, Entomology,Clinical Chemistry,, and Histopathology).
ii. Kufundisha wanafunzi na wafanyakazi waliochini yake
iii. Kufanya utafiti wa kimaabara ili kubaini mbinu nzuri za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali.
iv. Kuchukua sampuli zizonahitaji utaalamu maalum
v. Kuweka kumbukumbu sahihi za majibu ya vipimo katika rejista na katika mfumo Kutunza vifaa vya kazi na vitendanishi

**Sifa za Mwombaji**

i. Awe amehitimu shahada ya kwanza ya maabara kutoka vyuo vikuu vinavyotambulika na serikali na awe amehitimu mafunzo ya mwaka mmoja ya Intership.
ii. Awe amesajiliwa na Baraza la Maabara Tanzania
iii. Awe Raia wa Tanzania
iv. Awe na uzoefu katika masuala ubora wa maabara ( Quality Assurance activities)
v. Awe na uzoefu wa kazi wa miaka 3 na kuendelea ikiwemo uwezo wa kusimami wafanyakazi wengine.
vi. Awe ana ujuzi wa kutumia kompyuta

**1.8 Mteknolojia Daraja II ( Technologist II)( Maabara -2 na Mionzi-2, )- Nafasi 4**

**Kazi na Majukumu**

i. Kufanya kazi za uchunguzi katika fani yake ya kazi.
ii. Kufundisha wanafunzi na wafanyakazi waliochini yake.
iii. Kufanya utafiti ili kubaini mbinu nzuri za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali.
iv. Kuweka kumbukumbu sahihi za majibu ya vipimo katika rejista na katika mfumo Kutunza vifaa na vitendea kazi .
v. Kutunza mitambo, vifaa na mali zote zilizopo katika idara yake

**Sifa za Mwombaji**

i. Awe amehitimu stashahada ya fani husika (maabara au mionzi) kutoka vyuo vinavyotambulika na serikali.



KNY MKURUGENZI MTENDA
HOSPITALI YA RUFAA NKIN
S. L. P 1, NKINGA
TABORA

ii. Awe amesajiliwa na Baraza la Maabara au Mionzi Tanzania
iii. Awe Raia wa Tanzania
**iv.** Awe na uzoefu wa kazi wa miaka 2 na kuendelea .
v. Awe anaujuzi wa kutumia kompyuta

**1.9 Mteknolojia wa Macho II – Nafasi moja**

**Kazi na Majukumu**

i. Kutibu wa wagonjwa wa macho.
ii. Kufanya uchunguzi wa upeo wa kuona, kutibu na kutoa usauri nasaha.
iii. Kutengeneza miwani na kurekebisha miwani ya aina zote.
iv. Kutunza vifaa vya kazi.

**Sifa za Mwombaji**

i. Awe na amehitimu stashahada katika fani ya uteknolojia wa macho katika chuo kinachotambulika na serikali.
ii. Awe amesajiliwa na baraza la maabara la Tanzania.
iii. Awe na uzoefu wa kazi wa mwaka mmoja na kuendelea.
iv. Awe ana ujuzi wa kutumia kompyuta

**2. AJIRA ZA KUJITOLEA**

Hospitali inatangaza nafasi za ajira ya kujitolea kwa kada zifuatazo:

i. Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja II ( Assistant Nursing Officer II) – Nafasi 15
ii. Mteknolojia – Dawa daraja II ( Pharmaceutical Technologist II) - Nafasi 3
iii. Mteknolojia – Maabara daraja II (Laboratory Technologist II) – Nafasi 3
iv. Mteknolojia – Mionzi Daraja II ( Radiographer II) – Nafasi 2
v. Mteknolojia - Meno Daraja la II – Nafasi 1

**Sifa za Waombaji**

i. Wawe wamehitimu stashahada katika fani husika mwaka kati ya 2020 na 2021.
ii. Wawe wamesajiliwa katika mabaraza yanayohusiana na fani zao.
iii. Wawe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
iv. Wawe tayari kufanyakazi kwa kuzingatia kanuni na maadili ya kazi zao.
v. Wawe tayari kulipwa posho ya shilingi laki moja na nusu kwa mwezi.
vi. Hakuna uzoefu wa kazi unaohitajika .

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Waombaji wote watume barua za maombi na kuambatanisha na Maelezo ya Wasifu Binafsi(CV) , vivuli vya vyeti vya sekondari, Vyeti vya taaluma, vyeti vya kuzaliwa , Leseni , vyeti vya usajili, kitambulisho cha NIDA na vyote viwe vimethibitishwa na mwanasheria. Nyaraka zote ziwe katika PDF. Kumbuku kutaja Nafasi ya kazi unayoomba kwenye kichwa cha habari cha barua yako pamoja na kwenye Subject ya email unapotuma maombi yako(kwa wale watakaotuma kwa email). **Usikubali kutoa fedha/Rushwa ya aina yoyote kwa ahadi ya kupatiwa ajira. Ukiombwa fedha/rushwa toa taarifa 0754 830532 na 0784800098.**

**Barua zote za maombi ziandikwe na kutumwa kwa: Mkurugenzi Mtendaji, Hospitali Ya Rufaa ya Nkinga, S.L.P 1, Nkinga, Igunga, Tabora , Tanzania. Tel. +255 784800098 Email: nkinga-hospital@hotmail.com.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15 Oktoba, 2021 saa 10:30 jioni. Wale ambao hawatasikia kutoka kwetu baada ya wiki mbili kutoka tarehe ya mwisho wa kupokea maombi wajue kwamba hawakuchaguliwa.

KNY MKURUGENZI MTENDAJI
HOSPITALI YA RUFAA NKINGA
S. L. P 1, NKINGA
TABORA